



SURVIVAL HOSPITAL

A: Plot No. 1 Block D, Mabira Street | Kyerwa District, Kagera

T: +255 (0) 625083207 | +255 (0) 767710320 | +255 (0) 766 171158 | +255 (0) 757 021056

E: info@survival.co.tz | ndyamukama1989@gmail.com

W: <https://www.survival.co.tz>

YAH: TANGAZO LA KUITWA KUSAINI MKATABA NA KURIPOTI KAZINI KUANZIA TAREHE 5 AGOSTI 2024 MPAKA 9 AGOSTI 2024

Mpendwa Mtumishi,

Hospitali ya Survival inapenda kukutangazia kuwa kama ulipigiwa simu/ulitumiwa email kutaarifiwa kuwa umechaguliwa kuwa mionganini mwa watumishi wa Hospitali ya Survival, unataarifiwa kuwa kwa kipindi cha kuanzia tarehe 4 Agosti 2024 mpaka tarehe 9 Agosti 2024 tutakuwa na zoezi la kusaini mikataba ya ajira na kuchukuwa vipimo kwa ajili ya ununuzi wa sare(uniform) za hospitali kwa watumishi. Hivyo unaombwa kufika katika vituo vifuatavyo.

1. OFISI ZA GEITA (SURVIVAL PHARMACY)

WAFAMASIA NA PHARMACEUTICAL TECHNICIAN mnaombwa kufika katika Ofisi za Survival Hospital zilizopo Geita katika Mtaa wa Uwanja, Kata ya Nyankumbu, Jengo la Furahisha kuanzia kesho tarehe 1 Agosti 2024. Mara baada ya kusaini mkataba, mtaanza kazi ya kuhakiki dawa zilizopo stoo na kuzipeleka Hospitalini kabla ya tarehe 9 Agosti 2024. Kwa muda wote uwapo Geita kabla ya kwenda Hospitalini Ofisi itagharamia sehemu ya kuishi (accommodation). Au Piga simu kwa maelezo **0767710320** au **0766 171158**.

2. OFISI YA MKURUGENZI WA UTAWALA KATIKA HOSPITALI YA SURVIVAL

KADA NYINGINE TOFAUTI NA ZILIZO TAJWA HAPO JUU Unaombwa kufika Hospitalini kuanzia tarehe 4 Agosti 2024 mpaka tarehe 9 Agosti 2024 kusaini mkataba. Anuani ya kufika hospitali ni kama ifuatavyo:-

Kutokea Mikoa Mingine hakikisha unafika Mkao wa Kagera. Na ufikapo Mkao wa Kagera hakikisha unaenda mpaka Wilaya ya Karagwe katika Mji wa Kayanga au Omurushaka.

Ukiwa Mji wa Kayanga Utapanda magari ya kuelekea Mabira kuitia Rwambaizi (**Takribani 52km**). Ukifika Mabira Ulizia Hospitali Mpya ya Survival Hospital utaweza kufika bila shida. (**Ipo 2km kutoka Mabira Centre**) Au Piga simu kwa maelezo zaidi **0767710320** au **0762 120540**

Ukiwa Mji wa Omurushaka, Panda magari ya kuelekea Mji Mdogo wa Nkwenda (**Takribani 37Km**) Ukiwa Nkwenda panda magari ya kuelekea Mabira (Takribani 33km). Ukifika Mabira Ulizia Hospitali Mpya ya Survival Hospital utaweza kufika bila shida (**Ipo**

2km kutoka Mabira Centre). Au Piga simu kwa maelezo **zaidi 0767710320** au **0762120540**

Ukiwa Mji wa Kayanga ila ukahitaji kuitia Nkwenda, panda daladala za kutokea Kayanga kwenda Omurushaka. Kutokea Omurushaka tumia anuani tajwa hapo juu kufika Hospitalini. Hata hivyo waweza tumia **Google Map** kwa kuandika neno Mabira-Kyerwa kisha fuata ramani

Baada ya kusaini mkataba utaambiwa ni tarehe ipi unapaswa kuripoti kazini. Siku ya kusaini mkataba, chai ya asbuhi, maji ya kunywa na chakula cha mchana mtalipiwa na Ofisi kwenye Mgahawa wa Hospitali.

3. MUHIMU

Hakikisha unakuja na vifuatavyo kwa ajili ya kufungua jalada lako la ajira.

- i. Vyeti vyako original, na nakala yake kwa ajili ya kuweka kumbukumbu.
- ii. Leseni yako ambayo haijaisha muda wake na nakala yake.
- iii. Kitambulisho cha NIDA au nakala yake
- iv. Picha ndogo 3 (passport size)
- v. Taarifa zako za benk (tunapendekeza CRDB, ukiwa huna CRDB waweza leta akaanti ya Benk nyingine), TIN namba kama unayo, NSSF namba kama unayo kwa ajili ya update za payroll. Pia kumbuka watu wako wa karibu (next to keen)
- vi. Usitoke hospital bila kuchukuwa vipimo vyta sare kwa watumishi ambao hulazimika kuva sare muda wote wawapo kazini.
- vii. Wakuu wa vitengo kupewa nyumba za kukaa ambazo mtapewa bure na hospitali hata hivyo mtalazimika kuacha funguo za nyumba hizo sehemu mtakazo elekezwa na kuzichukua pale mtakapo kuja kuripoti kazini.
- viii. Kwa watumishi wengine ambao hospitali haitawapa nyumba za kuishi mtaunganishwa na mtu ambaye atawasaidia kupata nyumba za kuishi kwa bei nafuu pale mtakapo ripoti kazini. Hata hivyo mpango wa muda mrefu wa hospitali ni kuhakikisha kwa kipindi cha miaka 3 ijayo watumishi wote wanaishi bure kwenye nyumba za hospitali (*Kwa watakao Penda*).

Uongozi wa Hospitali unachukua nafasi hii kuwakaribisha sana katika taasisi yetu huku tukiamini kuwa hii ni ya kwetu sote. Nyie ni watu muhimu sana kuifanya taasisi hii in kuwa na kufikia malengo.

“SISI NI SEHEMU YA TUMAINI JEMA”

KARIBU SANA

**BURHAN K. RUTENGE
MKURUGENZI WA UTAWALA
HOSPITALI YA SURVIVAL**